

**TAARIFA YA MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB), WAZIRI WA  
NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU) KUHUSU  
KUWASILISHWA BUNGENI KWA TAARIFA YA HALI DAWA ZA  
KULEVYA YA MWAKA 2021**

---

**Ndugu Wanahabari,** Leo tarehe 10 mwezi Juni mwaka 2022, nimewasilisha mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya nchini ya mwaka 2021 ili kutekeleza matakwa ya Kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015. Kifungu hicho kinaweka masharti kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuandaa na kuiwasilisha bungeni kila mwaka taarifa ya hali ya dawa za kulevya nchini.

Lengo la taarifa hii ni kuwafahamisha wananchi hali halisi ya tatizo la dawa za kulevya kitaifa na kimataifa, jitihada zilizofanywa na Serikali na taasisi zake katika kukabiliana na tatizo hili, ushirikiano uliopo kati ya Nchi yetu na Nchi zingine katika kudhibiti na kupambana dawa za kulevya, pamoja na changamoto zilizopo katika kukabiliana na tatizo hili.

**Ndugu Wanahabari**, Serikali imeendelea kupambana na tatizo la uzalishaji, matumizi na biashara ya dawa za kulevyo Nchini. Kama ilivyokuwa katika kipindi kilichopita uzalishaji, matumizi, biashara ya dawa za kulevyo imeendelea kuwa tatizo duniani na kuleta athari za kiuchumi, kijamii na masuala ya ulinzi na usalama.

Bangi na mirungi zimeendelea kuwa tatizo Nchini. Katika mwaka 2021, jumla ya tani **22.74** za bangi zilikamatwa, ikiwa ni ongezeko la asilimia **72** ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2020. Ukamataji huu ulihusisha jumla ya watuhumiwa **9,484**. Mirungi iliyokamatwa katika kipindi hicho ilifikia tani **10.93** zikihusisha watuhumiwa **1,395**.

Aidha, Kwa upande wa dawa za kulevyo zinazozalishwa viwandani, mwaka 2021 jumla ya **tani 1.13** za heroin zilikamatwa. Hiki ni kiasi kikubwa kuwahi kukamatwa kwa mwaka mmoja katika historia ya nchi yetu. Kiasi hicho ni mara tatu ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2020. Aidha, katika kipindi hicho kiasi cha gramu **811.30** za cocaine zilikamatwa.

**Ndugu Wanahabari**, kwa mara ya kwanza mwaka 2022, katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevyta Nchini, shehena kubwa ya jumla ya kilo **430.77** za dawa za kulevyta aina ya methamphetamine inayotengenezwa na kemikali bashirifu ilikamatwa, ikihusisha watuhumiwa tisa raia wa Iran wote wakiwa wanaume. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali inaendelea kufuatilia mwenendo wa uingizwaji na matumizi ya methamphetamine pamoja na kemikali bashirifu ambazo hutumika kutengeneza dawa hizo.

Tatizo la matumizi ya dawa za kulevyta nchini limeendelea kuwepo pamoja na juhudhi za udhibiti zinazofanywa na serikali. Hadi kufikia mwezi Desemba 2021, waraibu wa dawa mbalimbali za kulevyta pamoja na vilevi vingine wapatao **905,902** walijitokeza kupata tiba katika hospitali za wilaya na mikoa nchini.

**Ndugu Wanahabari**, Serikali imeendelea kupanua wigo wa matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevyta ambapo hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 huduma za tiba ya uraibu zilikuwa zikipatikana kwenye vituo 15 vya kutolea tiba kwa waraibu wa heroini (MAT Clinics) na vituo hivi kwa pamoja vilikuwa vimesajiri waraibu **11,650**. Vituo hivi vinapatikana katika mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Tanga, Mbeya, Songwe, Dodoma, Mwanza na Arusha.

Serikali imeendelea kufanya usimamizi katika nyumba **44** za Upataji Nafuu (Sober House) nchini. Nyumba hizi huanzishwa na kuendeshwa na asasi za kiraia na Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imetengeneza Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Upataji nafuu nchini. Mwongozo huu unasaidia kuzifanya nyumba hizi kutoa huduma za utengamao kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

**Ndugu Wanahabari**, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na wadau wote kwa ushirikiano uliowezesha udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika mwaka 2021 pamoja na kuhamasisha jamii kukabiliana na tatizo hili ambalo ni hatari kwa mustakabali wa nchi yetu. Aidha, napenda kuwahimiza wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali katika kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa manufaa yetu sote, ikiwemo kutumia simu ya bure namba **119** ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

George B. Simbachawene (Mb.).

**WAZIRI WA NCHI - OFISI YA WAZIRI MKUU  
(SERA, BUNGE NA URATIBU)**